JUA
GAZETI LA MAENDELEO

Kiongozi: Mutiri-wa-Bashara - Mwaka wa 22 - Toleo la 451

Taifa

# Mobutu ahitaji waziri mkuu mpya tarehe 12 januari '94

Katika hotuba yake ya tarehe 4 januari '94 kwa raïa ya inchi ya Zaïre kwa jumla Raïs Mobutu alisema kama atafanya yote iwezekanayo ili waziri mkuu mpya atakayeongoza serkali ya mpito ajulikane mbele ya tarehe 12 januari '94. Tarehe ifuatayo Birindwa anaweza akarushwe madarakani na kutiwa pembeni ili raïa waweze kupumua. Ni hivyo pya ametoa hitaji la ke kuona uchaguzi wa raïs mpya kama vile uchaguzi wa mabunge ufanyike mbele ya Desemba 31 ya mwaka huu tunao. Lakini magumu ni mengi inchini kufuatana na beyi ya vifaa, njaa, magojwa, ukosefu na matatizo mengi yaliyo letwa na mabadiliko ya pesa inchini mwetu. Pesa ya zaïre nyipya iliyoletwa na waziri mkuu Birindwa na iliyo pangwa jina ya "Yayote" yakataliwa sasa mjini Bukavu kufuatana na ukosefu wa pesa ndogo ndogo ama "Lumecha"..

Kweli, tangu hapo feza zetu zilizotolewa, matatizo mengi yakumba jamaa nyingi. Karibu pesa zilizotolewa na benki kuu ya taifa wakati wa mabadilisho zilikuwa noti za zaïres 100 ao 50. Noti hizo, machoni pa wachuuzi na wanunuzi hazikubaliwi haizuru na nani. Hivyo, wengi ulala na njaa ingawaje wanazo pesa. Tena yaonekana kuwa ikiwa mtu fulani aweza kuzikubali amlazimisha yule atakaye nunua kuweza kuuza vitu vya samani ya pesa zile zote.

Kwa mwisho watu hujiuliza sababu gani wakuu serkalini kafanya jambo kama lile ili waangamize kwa makusudi raia. Lakini tulipochunguza kwa makini tuliona labda kosa lile haliwahangukie kwa asili mia (100 %) wakuu wa serkali, bali hata wafanyakazi wengine.

Yesemakana kuwa mnamo tarehe 8/12/1993 wafanyabiashara na wafanyakazi wa Benki kuu ya Zaïre pa Bukavu kanaswa na walinda raia yaani "Gardes civiles" huko waliponaswa na saki kazaa za feza za hoti ya zaïres 1, 5 na 10 na zinginezo feza za kigeni. Huko wakishuhudia kuwa kwa nguvu zao binafsi hawawezi kupata feza hizo. Kwa hiyo ndugu hao kakanusha eti ni wakuu wao wa Benki walioamuru jambo lile. Baada ya siki moja, vita kazuka huko kamembe nchini Rwanda kati ya Wana-Zaïre na Wanyarwanda wakati hawakuelewana kwa bei ya kubadili pesa. Vita hivyo kasababisha kufungwa kwa mipaka kati ya nchi hio mbili. Lakini wachuuzi wengine akina mama wanaopenda kuangamiza uchumi baina ya ule wa nchi ya Rwanda kaziba masikio na kuvuka mipaka hapo walipojiletea matatizo ya kufyaturiwa masasi. Watatu kati yao kafariki dunia na wengine kajeruiwa vibaya. Kufuatana na hali hiyo, raia, kaingiwa na hasira na kuenda kuzingira nyumba ya benki kuu mnamo saa kenda za mchana kati, tarehe 10/12/1993, kusudi wabadili noti kubwa kwa zile ndogo. Jambo lililosimamiwa na askari jeshi pamoja na wakuu wa walinda raia, ambao wafanyakazi wa benki kawabadili yapata tu zaïres 300. Sikitiko ni kuona watu huangaika wakati wanayo haki ya kupata feze bila matatizo. Huruma kwa wanainchi hauko ndani ya viongozi wa mashirika kazaa na wachuuzi pia na wanasiasa.

UHARIRI

# Mwaka mpya na mambo mapya !

Ouf ! Mwaka wa 1993 umekwisha. *Tutasherehekea huu wa 1994, katika shangwe na vigelegele tukimsifu Mweny'Ezi Mungu. Mahitaji yetu uwe wa heri na fanaka.*

Kweli, mwaka wa 1993 kwa watu wengine ulikuwa wa kilio na wa matatizo mengi. Lakini umepita kama umeme kwa wenyi walikuwa na raha na kwa wengine kama kinyonga ukibeba mzigo wa magumu. Mauaji, wizi, njaa, magonjwa na mengineo magumu katuangamiza.

Mambo hayo yote yalipita mwakani 1993, mengi yaliweza kugunduliwa ama kupashwa katika nakala la Gazeti lenu tukufu "JUA" ao kuvisikia kwa wenzi wenu.

Katika jimbo letu la Kivu ya Kusini ingawa viongozi walipima kuhusika na kutia ukimya, ukingo wa usalama na uhusiano bora upashwao kuweko kati ya nchi jirani na rafiki kwa namna yao na kuhusika na afia ya wakaaji, mimonyoko ya arzi na uharibifu wa mabarabara kutokana na mafuriko ya maji ya mvua hata kuwatia jamaa kazaa wa kazaa katika vilio na mengineo magumu iliaangamiza raïa.

Nchini, mabadiliko muhimu kafanyika katika siasa. Serkali kazaa kasimikwa. Wanasiasa hawakuelewana na misukosuko yatezamiwa kutia uwasiwasi katika ujio wa nchi. Maandamano mengi yalifanyika katika umma kwa kuonya malalamiko na umaskini wa raïa. Ujeuri, chuki la kikabila, mauaji, uwizi, kubomolewa kwa makao, viwanda na maduka na vinginevyo vitendo vya ukaidi na vya uyanguyangu. Hayo yatia nchi katika miporomoko ya mateso raia wasijua la kufanya. Siasa ya uchumi, ya kijamii, ya usalama ikazorota. Ugonjwa wa Sida umetia vitisho siyo nchini tu bali pia ulimwenguni kote kutokana na idadi ya wagonjwa na waliofariki dunia.

Barani Afrika, serkali kazaa kapinduliwa, wakuu kuuawa ama kutiwa nguvuni na wengine kupingwa baada ya machaguzi na wengine kukimbia hadi nchi za kigeni. Huko Afrika ya Kusini wazungu na weusi wamesikilizana ikingojelewa uchaguzi kidemokrasia mwaka 1994.

Barani Azia, vita vimetezamiwa. Lakini iliyokuwa jambo la kusisimua ni kuona Wa-Palestina na Wa-Israeli kusikilizana na Wa-Palestina kupewa yao miji, mahali ya kuishi pahali pa kutangatanga duniani kama vipepeo.

Je, si mungelisahau kuwa Gazeti lenu " JUA " limetimiza miaka 21 mnamo tarehe 17 Novemba mwaka 1993 ? Kiongozi wake mhariri, bwana Mutiri-wa-Bashara, waandishi wake wote, ingawa umoja kafungwa gerezani kwa kusema ukweli kutokana na maandishi yao, na watumishi wake wote walifanya vyote wawezavyo ili wana-nchi wafuate kila iwezekanavyo mambo yaliyopita mijini, jimboni, nchini na mahali mengi ulimwenguni. Basi sisi wote twawatakia wasomaji mwaka huu wa 1994 uwe kweli wa heri, wa fanaka na wa ustawi.

André Bisimwa L-B. Tserou

# "Yayote" ni pesa mbaya

Siku hizi jimboni mwa Kivu ya kusini kwa jumla na mjini Bukavu kwa upekee njaa yawatesa wakaaji wanazaïre kama vile wageni.

Njaa kali inayowakumba na kuwagondesha watu wengi yatokana na ukosefu wa pesa ndogondogo ya noti ya pesa inayoitwa "Zaïre nyipya" ama"nouveau zaïre". Ijapokuwa chakula yapatikana mahali popote sokoni na madukani, pesa kubwa ya zaïre nyipya ya samani kubwa zaidi, ni kusema noti za 50 NZ na 100 NZ zakubaliwa na wachuuzi kwa shida. Mara na mara hao wachuuzi kama vile pia viongozi wa mashule, mahospitali na dispanseri, wasimamizi wa makanisa kazaa na mashirika ya usafirishaji na ya ununuaji wa madini na mafuta ya taa, wakataa noti hizo kubwa.

Noti hizo kubwa jameni, zimepewa majina mengi kwa sasa : Yayote, Masumbuko, Tabu ya Birindwa, na huko Uvira "Bikomago" ao damu ya Ndadaye na kazalika. Yaonekana kama magumu ya wanainchi wa Zaïre yaendelea kusababishwa na hali mbaya ya kiuchumi inchini na pia kulingana na mipango yakubadirisha pesa yetu kama zilivyokamatwa na waziri mkuu Fostino Birindwa. Lakini pia kufwatana na roho mbaya ya wachuuzi wanao pupa kali ya pesa na nia ya kuwina haraka kimagendo na kwa njia ya wizi na uuaji. Angalieni leo chupa la pombe "Primus" lauzishwa kwa bei ya 75 NZ na kesho pengine kwa bei kali ya 100 NZ ama milioni mia tatu ya zaïre za zamani !

Je, ni namna gani twaitaji kuingia ndani ya udemokrasia na katika inchi mpya ya haki na usawa ? Kwa nini wanazaïre hawamuogopi mwenyezi Mola anayewapatia baraka na bahati yakuishi katika utajiri kiroho na kimwili?

Kwa mwaka mpya 1994, wanazaïre wangejifunza namna gani kuheshimu na kumsaidia ndugu, jirani na binadamu wote, mwanainchi kama vile mgeni. Kufwatana na njia ya uhaki pahali pakuishi, katika ubaguzi wa rangi, wa kabila ao wa lugha.

Kutupilia mbali pupa ya pesa inayotuma wasemaji wa sheria na wenzio wasimamizi wa mahakma kuacha uhaki nakutupa gerezani wandungu wao wasiowapatia rushwa ingawa hawashtakiwe na kosa lolote. Inchini Zaïre haki ya binadamu yazarahuliwa.

Majina kama vile "yayote", masumbuko, mahangaiko zilizopewa na watu kwa noti mpya ya 50 NZ na 100 NZ zina maana mengi sana. Ni alama wazi kama watu wanateswa kufuatana na mabadiliko ya pesa iliyofanyika na waziri mkuu Faustino Birindwa.

# Udemokrasia, amani na chakula

Mchoko ao kazarau ? Hiyo ni ulizo lafikia wengi wanaojifikiri juu ya hali ya kisiasa iliyoko kwa sasa nchini Zaïre. Kwa kweli ukimya wa hasira waonywa na raïa tangu wanasiasa hawafikilie kuelewana na kukubaliana kuhusu uongozi wa nchi kama waweza siku moja kufikilia furaha kubwa ama hasira ya ajabu ikiambatana na matukio mazuri ama mabaya ya mikutano ya masikilizano yaendeshwa kati ya mabingwa wa vyama vya kisiasa na ambayo yaendeshwa tangu miezi kazaa sasa kusiwe tukio la kusisimua ao la tumaini. Leo hii vyama vyamuunga mkono Raïs wa Jamhuri vyatia mkwazo wa kukubali yote kahitajika na vyama vya upinzani mkali na wafuasi ila jambo moja tu halikubaliwe. Ni hilo la kumuinua bwana Etienne Tshisekedi kwenyi wazifa wa uwaziri mkuu wa serkali ya mpito.

Kwa ngambo yao, raïa waomba wanasiasa wawe na moyo wa mapendo kwa taifa lao na kwa ndugu zao wananchi wote. Wote twahitaji amani istareheshwe nchini. Lakini amani yaweza kuweko kweli kama wakaaji wapata vyakula na vinginevyo vifaa wanavyo lazima pia uhaki usimikwe halali. Kwani iwezekana je kusimulia juu ya amani na vyakula katika nchi ambamo sheria haiheshimiwe ? Hiyo ingefikilia tu vurugo nchini na kila mtu kufanya apendacho.

Kuambatana na maoni ya raïa kama vile mengineo taifa, tukio bora na la heri kuhusu mikutano kati ya wanasiasa kunako Jumba la Raïa litafanikiwa ni kama tu ukomo wa masikilizano na maelewano kati yao ndio uwe mbele ya yote. Kusiwe mshindi wala aliyeshindwa. Hiyo kweli ni maoni yetu katika kitumaini kitakachoendelea kuwaongoza wote ambao washurulila na mikutano hiyo. Ndugu wanasiasa wapaswa kusikia kama sio utafuti wa kupata cheo ama kiti cha uwaziri, kwa namna yoyote, ndicho kitendo chapaswa kuilaza na kuisaga amani na uhaki halali.

Ndiyo kusema yafaa kulinda makubaliano katukia kunako Mkutano mkuu wa kitaifa ambayo yaweza kusahishwa kama muna makosa lakini ikiambatana na njia iliyo halali. Na baadae kuomba kwa wananchi kujiweka kazini na mwishoe kukubali kama wananchi Mobutu na Tshisekedi ama mwakilishi wake wapaswa kutumika mkono mkononi. Na wote pamoja bila uwasiwasi kwa kuendesha namna iliyo bora serkali ya mpito bila kupendana lakini katika heshima ya hati zilizosimikwa. Hiyo ikiwa na faida moja, uchunguzi wa kila mmoja kwa mwengine, msinji wa uongozi bora wa mambo yaelekea umma. Kuenda kinyume cha mahitaji hayo ni kutia nchi katika shimo la moto. Kitendo ambacho hakuna mtu ahitaji. Twawaza sisi kama si vema kutia nchi katika hali mbovu ya misukosuko. Zamiri ikitusonga kuhusu hatari yatezamiwa kwa kuiteka nchi nyara, twawaomba hao vibeberu vigeni vya Barani Ulaya na Amerika ambavyo vina feza nyingi kutochochea na kuwasukuma ndugu zetu wanasiasa kutumbukia katika makosa ya zamani kwa kufikia faida zao wenyewe na kutupilia mbali heri ya ndugu zao raïa.

Kitumaini chetu nikuwa wote wa pande zote mbili, za mabwana Mobutu na Tshisekedi, wasikie na wakubali kama amani nchini itategemea masikilizano na maelewano yapaswa kuweko ili kulinda amani, vyakula kupatikana kwa uwingi na uhaki kustareheshwa kihalali. Hiyo ni mahitaji ya kila mmoja.

Basi, kwa kweli, kama mambo yanaongoka, hapo siku za usoni, wote watafurahiwa na kufurahishwa nchini na ulimwenguni kwa ujio bora wa nchi iliyo tajiri lakini ambamo raïa wamekuwa maskini ajabu kutokana na kuzorota kwa siasa ya uongozi, ya kiuchumi na ya kijamii kwa namna ya pekee.

André Bisimwa L-B. Tserou